**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**MHESHIMIWA RAHMA KASSIM ALI (MBM)**

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MEI, 2021**

# YALIYOMO


YALIYOMO....................................................................i

ORODHA YA VIAMBATANISHO....................................................iii

A. UTANGULIZI. ..............................................................1

B. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KUTUMIA MFUMO WA PROGRAMU KWA KIPINDI CHA JULAI, 2020 – MACHI, 2021.........................................4

B.1. PROGRAMU YA KWANZA: MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI. ...............................................4

B.1.1. Programu Ndogo ya Kwanza: Usimamizi wa Usafirishaji. ..............................................................5

B.1.2. Programu Ndogo ya Pili: Miundombinu ya Usafirishaji. ..............................................................10

B.1.3. Programu Ndogo ya Tatu: Huduma za Usafirishaji. ..............23

B.2. PROGRAMU YA PILI: MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA) 24

B.2.1. Programu Ndogo ya Kwanza: Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA. ...............................................24

B.2.2 Programu Ndogo ya Pili: Usimamizi wa Huduma za TEHAMA. ..................................................................26

B.3. PROGRAMU YA TATU: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI......27

B.3.1 Programu Ndogo ya Kwanza: Utawala na Uendeshaji...........28

B.3.2. Programu Ndogo ya Pili: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara. ..................................................................29

B.3.3. Programu Ndogo ya Tatu: Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba. ...........................................................30

C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI KWA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2020 – MACHI, 2021 KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 PAMOJA NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022. ..............................................................31

C.1 SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR....................................31

C.2 SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR. ...........................................36

C.3. MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR. ....................38

C.4. MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR ................40

D. MASHIRIKIANO NA TAASISI ZA MUUNGANO .......................44

E. MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KATIKA SEKTA YA USAFIRISHAJI NA MAWASILIANO......................................45

F. MUELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA KILA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022. .................................................................46

G. VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 ......................................................46

H. MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU NA MALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.........................................47

H.1. PROGRAMU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI. ...............................................................48
H.1.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji ....................48
H.1.2. Programu Ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji ...............50

H.2. PROGRAMU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA). ....................................................................52
H.2.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA .....................................................................52
H.2.2. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Huduma za TEHAMA .....................................................................54

H.3. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA. ....................................................................55
H.3.1. Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji........................55
H.3.2. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ...........................................................56
H.3.3. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba .57

I. HITIMISHO .........................................................................57

J. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022. ..................59

## ORODHA YA VIAMBATANISHO


Kiambatanisho Namba 1A: Ukaguzi wa Vyombo vya Moto Julai 2020 - Machi 2021 .................61
Kiambatanisho Namba 1B: Ruhusa za Njia na Usafirishaji Julai 2020 - Machi 2021 .................61
Kiambatanisho Namba 1C: Utoaji wa leseni kwa madereva wanafunzi kwa kipindi cha Julai 2020 - Machi 2021..........................61
Kiambatanisho namba 2: Orodha ya Taasisi zilizoungwanishwa na Mkonga wa Mawasiliano kwa kipindi cha Julai, 2020 – Machi, 2021. .......................62
Kiambatanisho Namba 3A: Wafanyakazi waliopatiwa mafunzo ya muda mrefu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ............................63
Kiambatanisho Namba 3B: Wafanyakazi waliopatiwa mafunzo ya muda mfupi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ............................63
Kiambatanisho Namba 4: Matumizi ya kawaida na maendeleo kwa kila programu kwa kipindi cha Julai 2020 - Machi 2021 ..........64
Kiambatanisho Namba 5: Mapato yaliyokusanywa kwa Kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021....................................64
Kiambatanisho Namba 6: Idadi ya ndege zilizohudumiwa kwa kipindi cha Julai 2020 - Machi 2021 .............................................65
Kiambatanisho namba 7: Orodha ya kazi za matengenezo ya barabara zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kupitia Mfuko wa Barabara Zanzibar.....................65
Kiambatanisho Namba 8: Orodha ya Miradi inayotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ....................................67

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kazi za Kawaida na kazi za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

2. **Mheshimiwa Spika**, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki katika kikao hiki cha Baraza la Wawakilishi kinachojadili Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2021/2022.

3. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Zanzibar wa awamu ya nane na kuendeleza Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar. Kuchaguliwa kwake kuiongoza nchi hii ni ushahidi tosha wa mapenzi na imani walionayo wananchi kwake. Ni imani yangu kuwa busara, uadilifu na hekima alizonazo Mheshimiwa Rais ataliongoza Taifa hili kwa ustawi na mafanikio makubwa. Vilevile, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ujasiri wake wa kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa lengo la kuleta maridhiano na kuwaunganisha Wazanzibari wote na kuhakikisha amani, utulivu na mshikamano wa kudumu katika nchi yetu.

4. **Mheshimiwa Spika**, napenda nimpongeze Makamo wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman

Abdulla kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa mashirikiano na miongozo wanayonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya kazi za Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Aidha, nachukuwa nafasi hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuchaguliwa tena kuliongoza Baraza lako Tukufu kwa busara, hekima na uadilifu.

5. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa mkono wa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kufuatia kifo cha Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Aidha, napenda kutoa Mkono wa Pole kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi kufuatia kifo cha aliyekuwa Makamo wa Kwanza wa Rais Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad.

6. **Mheshimiwa Spika**, naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa kuniteua na kunipa wadhifa wa kuiongoza Wizara hii. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ya kukuza na kuendeleza miuondombinu ya usafirishaji na mawasiliano ili iweze kutoa mchango mkubwa katika kufikia maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kadhalika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa miongozo anayoitoa kwa Wizara hii katika utekelezaji wa majukumu tuliyopewa. Miongozo hiyo inasaidia sana katika kuongeza ufanisi wa kazi pamoja na kasi ya maendeleo ya Sekta zinazosimamiwa na Wizara hii. Naahidi kuendelea kufanya kazi kadri ya uwezo wangu kwa kushirikiana na Watendaji wote katika kufanikisha

majukumu tuliyokabidhiwa na Serikali na kwa ufanisi zaidi.

7. **Mheshimiwa Spika**, naomba nimalizie kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Mawasiliano na Nishati ya Baraza la Wawakilishi chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Mohamed Ahmada Salum, Mwakilishi wa Jimbo la Wananchi Malindi, kwa maoni, hoja, mapendekezo, ushauri na maelekezo ambayo yameisaidia sana Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku. Kamati hii ilipata nafasi ya kutembelea Taasisi na miradi mbali mbali iliyomo ndani ya Wizara hii na kutoa ushauri na maoni yenye lengo la kuimarisha utekelezaji wa majukumu yetu. Ushauri na maoni wanayotupatia, tunaendelea kuyafanyia kazi kwa vitendo kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara.

8. **Mheshimiwa Spika**, matayarisho ya bajeti hii yamezingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2050), Sera ya Usafiri Zanzibar (2008), Mpango Mkuu wa Usafiri Zanzibar (Zanzibar Transport Master Plan), Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (2013), Sera mbali mbali za Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020-2025), ahadi pamoja na maagizo mbali mbali yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar. Katika utekelezaji wa mipango hiyo, Wizara imezingatia vipaumbele vikuu vya Serikali ikiwemo Maandalizi ya ujenzi wa Bandari Shirikishi - Mangapwani pamoja na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara mbali mbali Unguja na Pemba ikiwemo Barabara ya Chake – Wete (km 22), Barabara ya

Finya – Kicha (km 8.8), Barabara ya Fumba – Kisauni (km 12), Barabara ya Kiuyu – Maziwang'ombe – Micheweni (km 7) pamoja na Barabara ya Jumbi Sokoni – Tunguu (km 4). Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha sekta ya usafiri wa anga kwa kujenga uwanja wa Ndege wa Pemba pamoja uwanja mdogo wa Kigunda - Nungwi.

## B. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KUTUMIA MFUMO WA PROGRAMU KWA KIPINDI CHA JULAI, 2020 – MACHI, 2021

9. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutekeleza Bajeti kwa Kutumia Mfumo wa Programu (PBB). Hivyo, taarifa hii ya utekelezaji ninayoiwasilisha imezingatia Programu za Wizara ambazo tuliziwasilisha katika Bajeti ya Mwaka wa fedha 2020/2021 na kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi – Zanzibar. Vile vile, taarifa hii inajumuisha utekelezaji wa malengo mbali mbali ya Taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi, 2021.

10. **Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo, kwa heshima sasa naomba uniruhusu kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Programu kuu tatu (3) za Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi, 2021 kama ifuatavyo:-

### B.1. PROGRAMU YA KWANZA: MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI

11. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu na huduma za usafiri zilizo bora, salama na

endelevu. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana ni kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za usafiri zilizo salama na endelevu. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu ya Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ina Programu ndogo tatu (3) ambazo ni; Usimamizi wa Usafirishaji, Miundombinu ya Usafirishaji pamoja na Huduma za Usafirishaji.

### B.1.1. Programu Ndogo ya Kwanza: Usimamizi wa Usafirishaji

12. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani pamoja na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar.

**MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI ZANZIBAR**

13. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji ina jukumu la kudhibiti usalama wa watumiaji wa barabara, utoaji wa huduma za usafiri wa barabara pamoja na kusimamia Kamati ya Kitaifa ya Usalama Barabarani. Aidha, katika kutekeleza majukumu hayo, Mamlaka inafanya shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto, kutoa leseni kwa vyuo vya udereva na walimu wao, kuwafanyia majaribio ya nadharia na vitendo madereva wanafunzi, kutoa ruhusa za njia na usafirishaji wa abiria na mizigo, kutoa beji za utingo na madereva pamoja na kutoa vibali kwa madereva wa kigeni wanaotaka kuendesha vyombo vya moto hapa Zanzibar.

14. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi, 2021, kazi zilizofanyika katika Programu hii ndogo kupitia Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ni kama ifuatavyo:-

a. **Ukaguzi wa Vyombo vya Moto:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imekagua jumla ya vyombo vya moto 36,554 Unguja na Pemba ili kuhakikisha kuwa vipo katika hali ya uzima na salama; Vyombo hivyo, sawa na asilimia 75 ya makadirio ya vyombo 48,900 vilivyopangwa kukaguliwa katika kipindi hicho. Kati ya vyombo hivyo, 30,832 vimekaguliwa Unguja na 5,722 vimekaguliwa Pemba. **Kiambatanisho namba 1A** kinahusika**.**

b. **Utoaji wa Ruhusa za Njia na Usafirishaji:** jumla ya ruhusa za njia na usafirishaji 10,126 kwa gari mbalimbali zinazotoa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo zimetolewa Unguja na Pemba. Kiwango hicho ni ongezeko la ruhusa za njia 1,017 kati ya 9,109 zilizotolewa kwa mwaka 2019/2020. Kati ya ruhusa hizo, 8,919 zimetolewa Unguja na 1,207 zimetolewa Pemba. **Kiambatanisho namba 1B** kinahusika**.**

c. **Utoaji wa Leseni kwa Gari za Biashara:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imefanikiwa kutoa leseni za usafirishaji wa gari za biashara aina mbali mbali zinazotoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo ambapo jumla ya leseni 8,612 zimetolewa sawa na asilimia 94 ikilinganishwa na leseni 9,150 zilizotolewa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/2020. Kati ya leseni hizo, 7,606 zimetolewa Unguja na 1,006 zimetolewa Pemba.

d. **Majaribio ya Madereva,** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imewafanyia majaribio ya nadharia na vitendo jumla ya madereva 9,731 sawa na asilimia 104 ya madereva 9,325 waliokadiriwa kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2020/2021, ikiwa ni ongezeko la madereva 38 ikilinganishwa na madereva 9,693 waliofanyiwa majaribio kwa mwaka 2019/2020.

e. **Utoaji wa Beji za Utingo na Madereva.** jumla ya beji 8,579 zimetolewa kwa utingo na madereva wa gari za biashara za aina mbalimbali sawa na asilimia 168 ya makadirio ya beji 5,100 zilizopangwa kutolewa katika kipindi hicho. Kiwango hicho ni sawa na ongezeko la beji 3,825 ikilinganishwa na beji 4,754 zilizotolewa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/2020. Kati ya beji hizo, 4,365 zimetolewa kwa madereva na 4,214 zimetolewa kwa utingo. Aidha, beji 8,105 zimetolewa Unguja na 474 zimetolewa Pemba.

f. **Utoaji wa Leseni za Madereva Wanafunzi:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imetoa leseni za kujifundishia vyombo vya moto kwa Madereva Wanafunzi 7,166 sawa na asilimia 69 ya makadirio ya leseni 10,390 zilizopangwa kutolewa katika kipindi hicho ikiwa ni upungufu wa leseni 2,225 ikilinganishwa na leseni 9,341 zilizotolewa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/2020. Kati ya Leseni hizo, 6,136 zimetolewa Unguja na 1,030 zimetolewa Pemba. **Kiambatanisho namba 1C** kinahusika**.**

g. **Utoaji wa Vibali kwa Madereva Wageni.** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi 2021 jumla ya vibali vya madereva wageni 10,689 vimetolewa sawa na asilimia 384% ya

makadirio ya vibali 2,787 vilivyopangwa kutolewa katika kipindi hicho.

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilikadiria kukusanya jumla ya TSH 3,400,585,000 na hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya TSH 2,102,551,400 zimekusanywa sawa na asilimia 61 ya makadirio.

**WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR**

16. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Karakana Kuu ya Magari imepewa jukumu la kuvifanyia matengenezo vyombo vya moto vya Serikali na binafsi kupitia karakana zake zilizopo Unguja na Pemba pamoja na kutoa ushauri wa ununuzi na uuzaji wa Gari za Serikali.

17. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi, 2021 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Wakala wa Karakana Kuu ya Magari imefanikiwa kutekeleza yafuatayo;-

a. **Matengenezo ya Gari:** Wakala imefanikiwa kuzifanyia matengenezo gari 801 ikilinganishwa na gari 588 sawa na ongezeko la gari 213 zilizotengenezwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Kati ya gari hizo, gari 663 ni za Serikali na 138 ni gari za watu binafsi.

b. **Utoaji wa Ushauri wa Manunuzi na Uuzaji wa Gari za Serikali:** Wakala imepokea maombi na kutoa ushauri kuhusiana na ununuzi wa vyombo vya moto kwa Taasisi nne (4) za Serikali ikiwemo Kamisheni ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Nchi (OR) Fedha na Mipango, Wizara

ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto. Aidha, kwa upande wa uuzaji wa vyombo vya moto, Wakala imepokea maombi na kutoa ushauri kwa Taasisi tatu (3) kuhusiana na uuzaji wa vyombo vyao. Taasisi hizo ni Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Wakala wa Majengo Zanzibar.

c. **Uimarishaji wa Karakana Unguja na Pemba:** Wakala inaendelea kuziimarisha Karakana zake zilizopo Unguja na Pemba kwa kuzifanyia matengenezo mashine nne (4) kubwa za magari katika Karakana Kuu zilizopo Chumbuni na Chake Chake ambazo hapo awali zilikuwa hazifanyi kazi. Lengo la kuzifanyia matengenezo mashine hizo ni kurahisisha utoaji wa huduma za matengenezo ya gari. Aidha, katika kuimarisha Karakana Kuu ya Pemba, Wakala imepeleka vifaa mbalimbali vya matengenezo ya gari katika Karakana hiyo zikiwemo mashine nne (4) za kutengeneza gari. Katika uimarishaji wa Karakana Kuu, Wakala imewajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kutoa mafunzo kwa vitendo kwa mafundi 18 Unguja na Pemba.

**18. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,186,900,000 kwa kazi za kawaida na mishahara. Kati ya fedha hizo, TSH 1,344,200,000 ni Ruzuku kwa ajili ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani na TSH 842,700,000 ni Ruzuku kwa ajili ya Wakala wa Karakana Kuu ya Magari. Hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH 952,681,372 zimetumika sawa na asilimia 43.5 ya makadirio ya bajeti ikiwa ni Ruzuku kwa kazi za kawaida na mishahara. Kati ya fedha hizo TSH

562,729,050 ni matumizi kwa ajili ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani na TSH 389, 952, 322 ni matumizi kwa ajili ya Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar.

### B.1.2. Programu Ndogo ya Pili: Miundombinu ya Usafirishaji

19. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Wakala wa Barabara Zanzibar pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Programu hii ina lengo la kuwepo miundombinu ya usafirishaji iliyo bora, salama na endelevu kwa Unguja na Pemba.

**WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR**

20. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia Programu ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji ina jukumu la kujenga, kutunza na kuzifanyia matengenezo barabara mbali mbali za Unguja na Pemba ili ziweze kupitika muda wote. Kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi, 2021 Wakala wa Barabara kupitia programu hii ndogo imefanikiwa kuzifanyia matengenezo barabara mbali mbali za Unguja na Pemba kwa kiwango cha lami kama ifuatavyo:-

a. **Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kinduni-Kichungwani-Kitope (km 4) kwa Kiwango cha Lami pamoja na Ujenzi wa Madaraja**

21. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ujenzi wa barabara hii unaendelea na hadi kufikia mwezi wa machi 2021, umefikia asilimia 80 ya utekelezaji. Aidha, jumla ya kilomita 3.2 zimekamilika kwa kiwango cha lami pamoja na kukamilisha ujenzi wa madaraja makubwa mawili katika barabara hiyo.

**b. Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Sharifumsa-Mwanyanya-Skuli ya Bububu (km 3.8) kwa Kiwango cha Lami**

**22.** **Mheshimiwa Spika,** kazi zilizofanyika hadi kufikia mwezi Machi 2021 ni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa urefu wa km 3.1, ujenzi wa makalvati na uwekaji wa mabomba yanayokatisha barabara (duct services) kwa ajili ya kupitisha mabomba ya maji safi. Mradi huu unatekelezwa sambamba na mradi wa ujenzi wa barabara ya Kinduni – Kichungwani - Kitope (km 4) ambao unajengwa kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi wa madaraja. Mradi huu unagharimu jumla ya TSH 8,146,017,004. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2021 mradi huu umefikia asilimia 82 na jumla ya TSH 3,614,922,497 zimepatikana sawa na asilimia 44.

**c. Mradi wa Ujenzi wa Barabara kutoka Daraja la Dk. Shein hadi Soko la Jumbi (km 1.1) kwa Kiwango cha Lami**

**23.** **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu umefikia asilima 75 ya utekelezaji na kazi zilizofanyika ni ujenzi wa tuta la barabara pacha upana wa mita 25, ujenzi wa kalvati moja, ujenzi wa kingo za zege zinazogawanya barabara (median) na ujenzi wa msingi wa maji ya mvua uliofunikwa kwa makalbi yenye urefu wa mita 300. Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,348,515,836 na hadi kufikia machi, 2021, jumla ya TSH 2,090,544,111 zimepatikana sawa na asilimia 89 ya makadirio ya bajeti.

d. **Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kipapo - Mgelema - Wambaa (km 9.3) kwa Kiwango cha Lami**

24. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unaendelea na kazi zilizofanyika ni usafishaji wa eneo la barabara, ujenzi wa madaraja madogo 11, ukataji wa vilima na uwekaji wa kifusi tabaka la kwanza na la pili kwa urefu wa km 6 kutoka Kipapo hadi Mgelema. Mradi huu umefikia asilimia 35 ya utekelezaji. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 800,000,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi ambapo fedha hizo zimepatikana.

e. **Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Maeneo Huru (Free zone) Micheweni (km 2.4) kwa Kiwango cha Lami**

25. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unajumuisha ujenzi wa tabaka la kifusi, kalvati, misingi pamoja na uwekaji wa lami. Kazi iliyofanyika ni uwekaji wa kifusi tabaka la pili kwa urefu wa km 2.4. Mradi huu unategemea kugharimu jumla ya TSH 1,610,000,000 na kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 300,000,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi na hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya TSH 200,000,000 zilipatikana. Mradi huu umefikia asilimi 48 ya utekelezaji.

f. **Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Michweni – Maziwang’ombe - Kiuyu (km 7.3) kwa Kiwango cha Lami**

26. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 100,000,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi na hadi kufikia machi, 2021

hakuna fedha zilizopatikana. Hata hivyo, Wakala wa Barabara Zanzibar Ofisi ya Pemba uliendelea na uwekaji wa beacons kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hiyo mara fedha zitakapopatikana.

g. **Matengenezo ya Barabara ya Mkiang'ombe (km 3.2) kwa Kiwango cha Kifusi**

27. **Mheshimiwa Spika,** Wakala ilipanga kuifanyia matengenezo barabara hii kwa kiwango cha kifusi. Hadi kufikia Machi, 2021, barabara hii imekamilika kwa asilimia 100 na kutumia jumla ya TSH 111,945,000 kutoka Mfuko wa Barabara Zanzibar.

h. **Matengenezo ya Sehemu ya Mangwena na Raha (Spot Improvement) katika Barabara ya Wete-Gando**

28. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipanga kufanya matengenezo makubwa sehemu zilizoharibika wakati wa mvua zilizonyesha mwaka 2017 na 2018 na kupelekea kukatika kwa mawasiliano ya usafiri katika barabara ya Wete - Gando eneo la Mangwena. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2021, kazi zilizofanyika ni kuondoa udongo na kuweka mawe na kifusi, kujenga Gabioni pamoja na kuweka lami katika eneo la Mangwena. Matengenezo ya barabara hii yalipangiwa kutumia jumla ya TSH 587,576,500 kutoka Mfuko wa Barabara Zanzibar kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 na 2020/2021 ambazo zimepatikana. Kazi za matengenezo ya barabara hii katika sehemu ya Mangwena zimefikia asilimia 95.

**i. Ujenzi wa Barabara Mbadala (Diversion) Eneo la Munguyupo na Changaweni kwa Kiwango cha Lami (km 0.72) katika Barabara ya Chake Chake - Mkoani**

**29. Mheshimiwa Spika,** Katika kuondoa changamoto ya usafiri iliyosababishwa na kukatika kwa barabara ya Mkoani – Chake Chake katika eneo la Munguyupo na Changaweni zilizosababishwa na mvua zilizonyesha mwaka 2017 na 2018, Wizara imejenga barabara mbadala (Diversion) katika maeneo hayo kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kupata huduma za usafiri kwa urahisi. Matengenezo hayo ya barabara mbadala yalipangiwa kutumia jumla ya TSH 197,560,000 kutoka Mfuko wa Barabara Zanzibar kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 na 2020/2021 ambazo zimepatikana.

**30. Mheshimiwa Spika,** vilevile, kazi za ukataji wa majani pembezoni mwa barabara, usafishaji wa misingi, makalvati pamoja na uzibaji wa mashimo kwa barabara za lami Unguja na Pemba zimefanyika.

**31. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia programu ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 3,404,700,000 kwa kazi za kawaida na mishahara. Hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH 2,387,529,010 zimetumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara sawa na asilimia 70 ya makadirio ya Bajeti. Kati ya fedha hizo, mshahara ni TSH 2,312,859,010 na matumizi ya kawaida ni TSH 74,670,000.

Aidha, kwa upande wa Mfuko wa Barabara Zanzibar, Wizara ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 11,360,000,000

na hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH 5,231,196,359 zimepatikana sawa na asilimia 46 ya makadirio ya fedha zilizopangwa.

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

32. **Mheshimiwa Spika**, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji ina jukumu la kuratibu na kusimamia miradi mbali mbali ya maendeleo katika sekta ya usafiri wa nchi kavu, anga na baharini pamoja na sekta ya mawasiliano. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Idara kupitia Programu ya Miundombinu ya Usafirishaji imesimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi ifuatayo:-

**B.1.2.1. MIRADI YA UIMARISHAJI WA USAFIRI WA BARABARA**

**a. Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Koani - Jumbi (km 6.3)**

33. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha ujenzi wa Barabara ya Koani – Jumbi yenye urefu wa km 6.3 kwa kiwango cha lami. Barabara hii imekamilika kwa asilimia 98 na ipo katika kipindi cha mwaka mmoja cha maangalizo. Barabara hii imejengwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) ikishirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, kazi ya ujenzi wa barabara hii imetekelezwa na Kampuni ya Mwananchi Engineering Constructing Company Ltd (MECCO Ltd) kutoka Tanzania ikisimamiwa na Wakala wa Barabara Zanzibar.

34. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2020/2021, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,000,000,000. Hadi kufikia Machi, 2021, hakuna fedha iliyopatikana kutoka BADEA na Serikalini.

b. **Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Bububu – Mahonda – Mkokotoni, Bububu Polisi – Kwanyanya, Pale – Kiongele, Matemwe – Muyuni na Fuoni – Kombeni (km 54.4)**

35. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unajumuisha ujenzi wa barabara ya Bububu – Mahonda – Kinyasini – Mkwajuni hadi Mkokotoni (km 31), Bububu Polisi hadi Kwanyanya (km 2.8), Pale – Kiongele (km 4.6), Matemwe – Muyuni (km 7.5) na Fuoni – Kombeni (km 8.5) zenye urefu wa km 54.4 kwa kiwango cha lami. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ikishirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Mradi huu tayari umeshakamilika kwa asilimia 100 na upo katika kipindi cha mwaka mmoja wa maangalizo.

36. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2020/2021, Mradi huu ulitegemea kutumia jumla ya TSH 9,834,300,000, kati ya fedha hizo, TSH 8,334,300,000 ni kutoka kwa Mshirika wa Maendeleo na TSH 1,500,000,000 kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH. 10,735,915,751 zimepatikana kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Aidha, hakuna fedha iliyopatikana kutoka Serikalini.

**c. Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Wete – Chake Chake (km 22.1)**

**37. Mheshimiwa Spika,** Wizara imepanga kuanza ujenzi wa barabara ya Wete – Chake yenye urefu wa km 22.1 kwa kiwango cha lami ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa barabara tatu za vijiji vya Kaskazini Pemba. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha za mkopo kutoka BADEA na SAUDI FUND ikishirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**38. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2020/2021, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 16,990,000,000, kati ya fedha hizo Jumla ya TSH 8,000,000,000 ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na TSH 8,990,000,000 kutoka BADEA na SAUDI FUND. Hadi kufikia Machi, 2021, hakuna fedha iliyopatikana katika mradi huu. Sababu kubwa ya kutokupatikana kwa fedha hizo ni kutokupatikana idhini ya kusaini mkataba wa Mkandarasi na Mshauri Elekezi (No objection) kutoka SAUDI FUND na BADEA.

**d. Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Fumba – Kisauni (km 12).**

**39. Mheshimiwa Spika,** Wizara imepanga kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Fumba – Kisauni ili kuweka miundombinu bora ya usafiri katika eneo la uwekezaji la Fumba na kuwawezesha wananchi kufikia huduma mbali mbali za kijamii na kiuchumi. Kwa mwaka wa fedha, 2020/2021, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH. 1,000,000,000 kutoka Serikalini kwa kukamilisha

kazi ya Upembuzi Yakinifu na kuanza kulipa fidia. Hadi kufikia Machi, 2021, kazi ya Upembuzi Yakinifu, Usanifu na Utayarishaji wa zabuni imekamilika na jumla ya TSH 400,000,000 zimepatikana kwa ajili ya malipo ya Mshauri Elekezi. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kutoka kwa washirika wa maendeleo.

e. **Upembuzi Yakinifu wa Barabara ya Kitogani – Paje, Mahonda - Donge, Kiyasini – Kiwengwa, Dunga – Chwaka, Muyuni – Nungwi na Makunduchi – Kizimkazi.**

40. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imepanga kuzifanyia Upembuzi Yakinifu barabara ya Kitogani – Paje, Mahonda - Donge, Kinyasini – Kiwengwa, Dunga – Chwaka, Muyuni – Nungwi na Makunduchi - Kizimkazi kwa lengo la kuzijenga upya, kuzitanua na kuziimarisha ikiwemo kuweka njia ya wanaotembea kwa miguu. Hadi kufikia Machi, 2021, kazi iliyofanyika ni kumpata Mshauri Elekezi ambayo ni Kampuni ya EDGE CONSULTANT kutoka Dar es Salaam. Mkataba wa kazi hiyo ulitiwa saini tarehe 8 Disemba 2020 kwa gharama ya TSH 1,581,012,253.60. Kazi ya Upembuzi Yakinifu imeanza na inatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi 18.

41. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2020/2021, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,000,000,000 kutoka Serikalini. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2021 hakuna fedha iliyopatikana.

f. **Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Jozani – Charawe - Ukongoroni (km 23)**

42. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaijenga Barabara ya Jozani – Charawe – Ukongoroni yenye urefu wa km 23 kwa kiwango cha lami. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ujenzi wa barabara hii unatekelezwa na Wakala wa Barabara Zanzibar. Hadi kufikia Machi, 2021, Kazi zilizofanyika ni uwekaji wa kifusi kilomita 1.3, usafishaji wa eneo la barabara (road corridor) kutoka Mapandani hadi Charawe Pwani, uwekaji wa lami ya kupika kilomita 2.5 pamoja na uwekaji wa lami ya maji kilomita 3. Aidha, kazi ya uwekaji wa kifusi inaendelea. Mradi huu umefikia asilimia 13 ya utekelezaji.

43. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2020/2021, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,000,000,000 kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya TSH 300,000,000 zimepatikana.

g. **Upembuzi Yakinifu wa Daraja la Uzi Ng’ambwa (km 2.2)**

44. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina lengo la kulijenga Daraja la Uzi Ng’ambwa ili kuwawezesha wananchi wanaoishi katika maeneo hayo kupata huduma za usafiri kwa urahisi zaidi. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kazi iliyofanyika ni kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu, Usanifu wa Kina (Detailed Design), uandaaji wa Michoro na utayarishaji wa zabuni pamoja na kuanza matayarisho ya ujenzi wa daraja hilo.

45. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2020/2021, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 5,000,000,000

kutoka Serikalini, hadi kufikia Machi 2021, jumla ya TSH. 274,000,000 zimepatikana.

### B.1.2.2. MIRADI YA UIMARISHAJI USAFIRI WA ANGA

a. **Mradi wa Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria (Terminal III) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA)**

46. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na juhudi zake za utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria (Terminal III). Mradi huu ulikuwa unatekelezwa kwa kutumia fedha za mkopo kutoka Benki ya Exim ya China pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hata hivyo, kutokana na kukosekana kwa fedha za ziada za ujenzi wa mradi huu kutoka Exim Bank, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kutenga fedha za ziada kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo ambalo linajengwa na Kampuni ya Beijing Construction Engineering Group Co. ltd (BCEG) kutoka nchini China na kusimamiwa na Mshauri Elekezi kampuni ya ADPi kutoka nchini Ufaransa.

47. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2021, kazi zilizofanyika ni pamoja na ufungaji wa samani (furniture) vikiwemo viti vya abiria, meza na viti vya ofisi, ufungaji wa mfumo wa usalama (CCTV camera), mashine za ukaguzi mizigo (X-ray machine), ufungaji wa mkanda wa kubebea mizigo ya abiria (conveyor belt), ujenzi wa maegesho ya gari (land side) pamoja na uwekaji wa mifumo mbali mbali katika jengo ikiwemo mifumo ya uhamiaji. Mradi huu umefikia asilimia 96 ya utekelezaji.

48. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2020/2021, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 130,086,073,000, kati ya fedha hizo, jumla ya TSH. 5,500,000,000 kutoka Serikalini, na TSH. 124,586,073,000 kutoka kwa Mfadhili. Hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH. 36,622,760,184 zimepatikana kutoka Serikalini ambazo zililipwa kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali.

**b. Uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba**

49. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina lengo la kuimarisha Uwanja wa Ndege wa Pemba kwa kuutanua na kuuongezea miundombinu ili kuwezesha kutua ndege kubwa na kutumika wakati wote. Kazi iliyofanyika ni utayarishaji wa michoro, nyaraka za zabuni (Tender Documents) pamoja na kuwatambua watakaoathirika kutokana na ujenzi wa mradi huo. Aidha, orodha ya watakaoathirika imeshawasilishwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanyiwa tathmini.

50. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH. 1,000,000,000 kutoka Serikalini kwa kazi za kuanza matayarisho ya ujenzi. Hadi kufikia Machi 2021, hakuna fedha iliyopatikana katika Mradi huu.

## B.1.2.3. MIRADI YA UIMARISHAJI USAFIRI WA BAHARINI

**a. Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri**

51. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipanga kufanya Upembuzi Yakinifu eneo la Mpigaduri kwa lengo la kujenga Bandari

mpya itakayohudumia mizigo inayoingia Zanzibar na kuwarahisishia wafanyabiashara katika utoaji wa mizigo yao kwa haraka na kuikuza Zanzibar kiuchumi. Kazi iliyofanyika ni kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu wa ujenzi wa bandari hiyo. Hata hivyo, kutokana na maamuzi ya Serikali kuhamishia ujenzi wa Bandari ya Mizigo katika eneo la Mangapwani, Mshauri hakuweza kuendelea na hatua ya usanifu na utayarishaji wa zabuni.

52. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2020/2021, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 5,000,000,000 kutoka Serikalini na hadi kufikia Machi, 2021 hakuna fedha iliyopatikana.

53. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kwa ujumla, Programu Ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 178,315,073,000. Kati ya fedha hizo, TSH 141,910,373,000 ni mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TSH 33,000,000,000 ni mchango kutoka Serikalini.

Aidha, jumla ya TSH 3,404,700,000 zilipangwa kwa matumizi ya kawaida ikiwa ni ruzuku kwa ajili ya Wakala wa Barabara Zanzibar. Hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya TSH 50,720,204,945 zimetumika sawa na asilimia 28.4 ya makadirio. Kati ya fedha hizo, TSH 10,735,915,751 ni mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 7.5 ya makadirio, TSH 37,596,760,184 ni mchango wa Serikali sawa na asilimia 113.9 ya makadirio na TSH 2,387,529,010 ni fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni ruzuku kwa Wakala wa Barabara Zanzibar sawa na asilimia 70.1 ya makadirio ya bajeti.

### B.1.3. Programu Ndogo ya Tatu: Huduma za Usafirishaji.

54. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya tatu ya huduma za usafirishaji inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ambayo ina lengo la kuwepo kwa huduma bora za usafirishaji wa abiria na mizigo baina ya Visiwa vya Zanzibar na maeneo mengine. Katika kufanikisha lengo hilo, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ilipanga kutekeleza mradi ufuatao:-

a. **Ununuzi wa Boti Ndogo za Abiria katika Maeneo ya Visiwa (Land Craft)**

55. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imepanga kununua boti 5 ambazo zitapelekwa katika visiwa vya Tumbatu, Fundo, Kojani, Kisiwapanza na Makoongwe kwa lengo la kuwapatia huduma bora na salama za usafiri wa baharini wananchi wanaoishi katika visiwa hivyo. Kampuni ya DAMEN SHIPYARDS kutoka Uholanzi imekamilisha kazi ya ujenzi wa boti hizo na zimeshawasili hapa Zanzibar.

56. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,500,000,000 kutoka Serikalini na hadi kufikia Machi, 2021, hakuna fedha iliyopatikana.

57. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu Ndogo ya Tatu ya Huduma za Usafirishaji ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,500,000,000 kutoka Serikalini na hadi kufikia Machi, 2021, hakuna fedha iliyopatikana.

## B.2. PROGRAMU YA PILI: MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

58. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma bora zenye kuendelea za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Zanzibar. Matokeo yanayotarajiwa ni kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za TEHAMA, ambazo zinachangia ukuaji wa Pato la Taifa la Zanzibar. Programu hii ina programu ndogo mbili ambazo ni; Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA pamoja na Usimamizi wa Huduma za TEHAMA.

### B.2.1. Programu Ndogo ya Kwanza: Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA.

59. **Mheshimiwa Spika**, programu hii inasimamiwa na Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar (ZICTIA) ambayo imepewa jukumu la kusimamia na kuendesha Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano wa Zanzibar, Kituo Kikuu cha Kuhifadhia Taarifa za Kielektroniki (Data Center) pamoja na kusimamia Minara ya mawasiliano ya simu. Programu hii ndogo ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu imara ya Mawasiliano iliyo salama na endelevu Zanzibar.

60. **Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi 2021, Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar imefanya matengenezo ya Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano katika maeneo ya Kibanda Maiti kwenye njia (Route) ya Mkonga iliyoanzia Jamhuri Garden hadi Amani pamoja na eneo la Barabara ya Koani – Jumbi kwa lengo la kurejesha huduma ya matumizi ya Mkonga huo baada

ya kutokea maharibiko yaliyosababishwa na harakati za ujenzi wa Barabara ya Amani pamoja na Barabara ya Koani – Jumbi. Aidha, matengenezo mengine ya Mkonga yalifanyika katika eneo la Kibonde Mzungu, Jumbi na Forodhani baada ya kutokea uharibifu wa Mkonga huo uliosababishwa na hujuma za makusudi katika maeneo hayo zinazofanywa na wananchi wasio wema.

61. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Pemba, matengenezo yamefanyika katika njia ya Chake Chake hadi Madungu ambapo Mkonga wa Taifa ulikatika kutokana na harakati za ujenzi wa mitaro ya barabarani katika maeneo ya Skuli ya Madungu Pemba. Vilevile, matengenezo yamefanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini - Pemba ambapo uharibifu wake umetokana na panya kukata baadhi ya nyaya za Mkonga huo.

62. **Mheshimiwa Spika,** Wakala imefanikiwa kuziunganisha na Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano Zanzibar jumla ya Taasisi za Serikali 28 kama zinavyoonekana katika **kiambatanisho namba 2.**

63. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Wakala pia imefanikiwa kuziunganisha na Kituo cha Kuhifadhia taarifa (Data Center) jumla ya taasisi mpya kumi. Taasisi hizo ni Kampuni ya Uvuvi ya Zanzibar (ZAFICO), Chama cha Watembeza Watalii Zanzibar (ZATO), Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Taasisi ya Uvuvi wa Bahari Kuu (Deep Sea), Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (ZFDA), Wakala wa

Serikali Mtandao Zanzibar, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar na Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF). Aidha, Wakala inaendelea kuimarisha mifumo ya umeme kwa kufunga "UPS" katika kituo kikuu cha kuhifadhia taarifa - Mazizini Zanzibar pamoja na kuimarisha vifaa vilivyomo katika kituo hicho.

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 1,760,000,000 kwa kazi za kawaida na mishahara ambazo ni ruzuku. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya TSH 553,530,835 zimetumika sawa na asilimia 31 ya makadirio ya Bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 280,200,835 ni Mshahara na TSH 273,330,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida.

### B.2.2 Programu Ndogo ya Pili: Usimamizi wa Huduma za TEHAMA.

65. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya pili ya usimamizi wa huduma za TEHAMA inasimamiwa na Idara ya Mawasiliano na ina lengo la kuhakikisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yanaongezeka kwa Taasisi zote pamoja na jamii.

66. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Wizara kupitia programu hii ndogo iliendelea kuratibu huduma za mawasiliano ya simu, intaneti pamoja na huduma za TEHAMA. Aidha, Wizara kupitia Idara ya Mawasiliano imefanikiwa kuimarisha mfumo wa mawasiliano kwa ajili ya matumizi ya Serikali kwa kuweka vifaa vya mawasiliano katika minara ya mawasiliano ya Serikali iliyopo Fumba kwa ajili ya kupokea na kupeleka

mawasiliano Tanzania Bara. Aidha, katika azma hiyo, mnara uliopo Nungwi nao umewekewa vifaa kwa ajili ya kupokea na kupeleka mawasiliano katika kisiwa cha Pemba pamoja na mnara wa Weles uliopo pembezoni mwa Jamhuri Garden kwa ajili ya kusambaza mawasiliano katika maeneo mbali mbali ya Unguja.

67. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kutumia wataalamu wake wa Idara ya Mawasiliano, imefanikiwa kutoa huduma na mafunzo ya TEHAMA kwa Masheha wote wa Unguja na Pemba kupitia Vituo vya TEHAMA Jamii ambavyo vipo katika Wilaya zote za Zanzibar. Aidha, wananchi wanashajihishwa kuhudhuria ili kupatiwa huduma na mafunzo yanayotolewa kupitia vituo hivyo.

68. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Huduma za TEHAMA ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 1,300,000,000 kwa matumzi ya kawaida na mishahara na hadi kufikia Machi 2021, jumla ya TSH 284,574,351 zimetumika sawa na asilimia 22 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo TSH 229,140,387 ni Mishahara na TSH 55,433,964 ni kwa kazi za kawaida.

## B.3. PROGRAMU YA TATU: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI

69. **Mheshimiwa Spika**, progamu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inatayarisha mipango bora na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii ina programu ndogo tatu ambazo ni:- Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara na Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba.

### B.3.1 Programu Ndogo ya Kwanza: Utawala na Uendeshaji.

70. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambayo imepewa jukumu la kusimamia uendeshaji wa Wizara na kushughulikia maslahi pamoja na nidhamu kwa wafanyakazi. Aidha, Idara inasimamia na kuandaa mpango wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi wa Wizara pamoja na uwekaji wa kumbukumbu za Wafanyakazi na mali za Wizara.

71. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, kazi zilizofanyika chini ya programu hii ndogo ni kuwajengea uwezo Wafanyakazi 18 kwa kuwapatia mafunzo mbali mbali ya muda mrefu na mfupi. **Kiambatanisho namba 3A na 3B** kinahusika. Aidha, wafanyakazi wapya 14 wamepatiwa mafunzo elekezi katika Chuo cha Utumishi wa Umma kwa lengo la kuelewa Sheria na Kanuni za kiutumishi. Pia, mazingira mazuri kwa watendaji yameimarishwa ikiwemo matengenezo ya Ofisi mbali mbali, kuimarisha vitendea kazi pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao nyengine. Mbali na hayo, Idara imeandaa mpango wa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa wafanyakazi wa Wizara kwa lengo la kuwa na utaratibu bora wa kuwajengea uwezo wafanyakazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

72. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,780,000,000 kwa kazi za kawaida na mishahara na hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH 875,838,394 zimetumika sawa na asilimia 32 ya makadirio ya Bajeti.

Kati ya fedha hizo, TSH 608,451,358 ni Mishahara na TSH 267,387,036 ni kwa ajili ya kazi za kawaida.

### B.3.2. Programu Ndogo ya Pili: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara.

73. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ambayo imepewa jukumu la kupanga, kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa sera, mipango, tafiti pamoja na miradi ya maendeleo katika Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji.

74. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaendelea kusimamia na kuratibu miradi mbalimbali ya maendeleo, kukusanya takwimu mbali mbali katika sekta za usafiri wa nchi kavu, anga na baharini pamoja na kutayarisha ripoti mbalimbali za utekelezaji wa kazi za Wizara. Aidha, Wizara imekamilisha kuandaa Mpango Mkakati mpya wa Wizara (Strategic Plan) ambao utatumika kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

75. **Mheshimiwa Spika,** Idara pia inaendelea kuratibu Taasisi na Mashirika yanayojitegemea yaliyo chini ya Wizara pamoja na kuratibu na kufanya vikao vitatu (3) vya ushirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ), Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (SMT) pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT).

76. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 924,000,000

kwa kazi za kawaida na mishahara na hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH 224,485,390 zimetumika sawa na asilimia 24 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 152,885,390 ni mishahara na TSH 71,600,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

### B.3.3. Programu Ndogo ya Tatu: Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

77. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Ofisi Kuu – Pemba ambayo imepewa jukumu la uratibu wa kazi za Wizara kwa upande wa Pemba. Kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni kuratibu na kusimamia shughuli zote za Wizara Pemba ikiwemo kuratibu kazi za utawala na utumishi, kazi za mipango na bajeti, usimamizi wa ujenzi wa barabara mbalimbali, huduma za usafiri wa barabara pamoja na huduma za TEHAMA.

78. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, programu hii ndogo ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 1,210,000,000 kwa kazi za kawaida na mishahara na hadi kufikia Machi, 2021, TSH 431,478,400 zimetumika sawa na asilimia 35.6 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 238,446,400 ni mishahara na TSH 193,032,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida.

79. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kupitia Programu zake kuu tatu (3) kwa mwaka wa fedha 2020/2021, iliidhinishiwa na Baraza lako tukufu kutumia jumla ya TSH 190,975,973,000 kwa kazi za kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH 54,042,793,687 zimetumika

sawa na asilimia 28.2 ya makadirio ya bajeti. Kati fedha hizo, TSH 48,332,675,936 ni miradi ya maendeleo na TSH 5,710,117,752 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ruzuku. **Kiambatanisho namba 4** kinahusika.

**UKUSANYAJI WA MAPATO**

**80. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ilipangiwa kukusanya jumla ya TSH 3,400,585,000 na hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH 2,102,551,400 zimekusanywa sawa na asilimia 61.8 ya makadirio ya mwaka. **Kiambatanisho namba 5** kinahusika.

## C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI KWA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2020 – MACHI, 2021 KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 PAMOJA NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

### C.1 SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR.

**81. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bandari lina jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji wa meli katika Bandari za Unguja na Pemba, ufungaji na ufunguaji wa meli kwenye gati, uangalizi wa alama za kuongozea meli (Minara na Maboya), uteremshaji na upakiaji wa bidhaa kwenye meli pamoja na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini.

**82. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi, 2021, Shirika limehudumia vyombo mbali mbali vya mizigo na abiria kupitia bandari zake za Unguja na Pemba vikiwemo meli za kigeni, meli za ndani pamoja na

majahazi, ambapo meli za kigeni zilizohudumiwa ni 100 zenye uzito wa GRT 1,097,821 ikiwa ni upungufu wa meli tatu sawa na asilimia 3 ikilinganishwa na meli 103 zilizohudumiwa katika kipindi cha Julai,2019 hadi Machi, 2020 ambapo idadi hiyo ya meli ni upungufu wa uzito wa meli GRT 243,879 sawa na asilimia 18 ukilinganisha na GRT 1,341,700 zilizohudumiwa katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020. Upungufu wa uzito huo unatokana na meli zilizohudumiwa kuwa na uzito mdogo pamoja na kutokuhudumiwa kwa meli za Kitalii na meli kubwa zenye uwezo kuanzia kuanzia TEUS 3000.

**83. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa meli za ndani, jumla ya meli 3,363 zilihudumiwa ikiwa ni ongezeko la meli 244 sawa na asilimia 8 ya meli za ndani zilizohudumiwa katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020. Aidha, jumla ya majahazi na boti za vyuma 5,201 zimehudumiwa katika kipindi hicho ikiwa ni ongezeko la majahazi 274 sawa na asilimia 6 ya makadirio.

**84. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa huduma za mizigo, Shirika limehudumia jumla ya tani 587,215 za mzigo wa meli ikiwa ni ongezeko la tani 235,913 sawa na asilimia 67 ya makadirio, ongezeko hili linatokana na mzigo wa saruji kuja kwa njia ya kichele badala ya makontena. Aidha, tani 75,172 za mzigo wa majahazi, pamoja na makontena 36,437 (sawa na TEUS 48,755) yamehudumiwa ikiwa ni upungufu wa makontena 10,366 (TEUS 12,872) sawa na asilimia 22 ya makadrio. Upungufu huo wa makontena umechangiwa kwa kiasi kikubwa na hali ya maradhi ya COVID-19, kupanda kwa gharama za usafirishaji pamoja na bei za bidhaa.

85. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi ya maendeleo, Shirika linaendelea kuimarisha vifaa vya kufanyia kazi bandarini ili kuongeza ufanisi wa kuhudumia mizigo na vyombo katika bandari zetu. Hadi kufikia Machi 2021, Shirika limetumia jumla ya TSH. 139,283,400 kwa ununuzi wa Gari ya kubebea wagonjwa ambayo hutumika kutoa huduma za dharura katika maeneo ya bandari. Aidha, Shirika lipo katika hatua za kufungiana mikataba na kampuni zilizoshinda zabuni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya bandarini ambavyo ni Reach Stacker moja, Terminal Tractor moja, Semi Teller moja na Winch Truck moja. Vifaa hivi vinatarajiwa kununuliwa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kupatikana kwa vitendea kazi hivi kutaongeza ufanisi wa utendaji wa kazi pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji.

86. **Mheshimiwa Spika,** Shirika linaendelea kuimarisha miundombinu yake kwa kuendelea na ujenzi wa Gati ya Mkokotoni ambapo kazi za ujenzi zimefikia asilimia 30. Aidha, ujenzi wa Jengo la Ghala la Malindi umekamilika kwa asilimia 100 na kutumia jumla ya TSH 996,889,958.

87. **Mheshimiwa Spika**, Shirika linaendelea kuimarisha Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA (ICT) na hadi kufikia Machi, 2021, Shirika linaendelea na hatua za kukamilisha taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuanza kazi ya kuandaa mfumo (E-Ports) ambao unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka fedha 2021/2022. Mfumo huu utakapokamilika, utaliwezesha Shirika kuongeza mapato kwa kupunguza mianya ya upotevu wa mapato, kupunguza matumizi yasiyo ya

lazima, kurahisisha upatikanaji wa taarifa za Shirika kwa wakati pamoja na kurahisisha huduma kwa wateja.

**Mapato na Matumizi**

88. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya TSH 37,536,536,678 na hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH 25,974,202,974 zimekusanywa sawa na asilimia 69 ya makadirio ya bajeti. Kwa upande wa matumizi ya kazi za kawaida, Shirika lilikadiria kutumia jumla ya TSH 30,536,334,423 na hadi kufika Machi, 2021 jumla ya TSH 13,085,752,127 zimetumika sawa na asilimia 43 ya makadirio. Aidha, Shirika limepanga kutumia TSH 6,980,000,000 kwa kazi za maendeleo na hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH 1,480,948,000 zimetumika sawa na asilimia 21 ya makadirio ya bajeti ambapo utekelezaji wa miradi hiyo umefikia wastani wa asilimia 38.

**MALENGO YA SHIRIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

89. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bandari kwa mwaka wa fedha 2021/2022 limepanga kuhudumia jumla ya meli 140 za kigeni zenye uzito (GRT) wa tani 1,670,000, meli za ndani zipatazo 4,200 na majahazi 7,300. Aidha, kwa upande wa huduma za mizigo, Shirika linatarajia kuhudumia tani 882,500 za mzigo mchanganyiko wa meli za ndani na nje, makontena 60,325 (TEUs 83,543), tani 157,273 za mafuta ya kuwasha (Petroleum Fuel) pamoja na tani 115,000 za mzigo wa majahazi.

**90. Mheshimiwa Spika**, Shirika limepanga kununua vifaa vya kufanyia kazi bandarini ambavyo ni mizani 4 za kupimia mizigo, Empty Reach Stacker moja, Terminal Tractor moja, Trailer moja, Mobile Crane moja (tani 100) pamoja na Mobile Harbor Crane moja (tani 125) pamoja na ununuzi wa Tishali (Barge) la kubebea mizigo. Kwa upande wa miundombinu, Shirika linatarajia kukamilisha kazi ya ujenzi wa gati ndogo katika bandari ya Mkokotoni pamoja na ujenzi wa Afisi ya Tawi la Shirika Pemba. Aidha, Shirika linatarajia kufanya Upembuzi Yakinifu kwa Bandari ya Wete, Wesha, Kizimkazi, Shumba mjini na Mkumbuu ikiwa ni hatua za awali za maandalizi ya ujenzi wa bandari hizo. Vilevile, Shirika linatarajia kuanzisha bandari kavu (ICD), kufanya marekebisho ya Jengo la Afisi ya Wesha pamoja na ununuzi wa "Fender" katika Gati ya Mkoani. Pia, Shirika linaendelea na uimarishaji wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) ambapo linatarajia kuweka mfumo wa E-port pamoja na mifumo mengineyo itakayosaidia kutoa huduma za bandari kwa urahisi.

**Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2021/2022**

**91. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Shirika la Bandari Zanzibar limepanga kukusanya jumla ya TSH 42,478,968,506 na kutumia jumla ya TSH 26,924,114,636 kwa kazi za kawaida na TSH 20,230,000,000 kwa kazi za maendeleo.

## C.2 SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR.

92. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Meli limepewa jukumu la kuzisimamia na kuziendesha meli zote za Serikali pamoja na kutoa huduma za Uwakala kwa meli za kigeni zinazoingia katika bandari za Zanzibar.

93. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Meli ya MV Mapinduzi II ilisita kutoa huduma kwa sababu ya kupata hitilafu za kiufundi. Wizara kwa sasa inaendelea kutafuta njia bora zaidi ili meli hii iweze kufanya shughuli zake kama kawaida. Aidha, Meli ya MV Maendeleo ipo chelezoni Mombasa kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo makubwa ikiwemo ubadilishaji wa mashine zake (Main Engines) mbili kubwa, vinu vya umeme (Generators) vyote viwili pamoja na ubadilishaji wa “plates” zilizochakaa. Kazi za matengenezo ya umbile la meli (steel works) zimekamilika kwa wastani wa asilimia 75 na kazi iliyobaki ni ufungaji wa mitambo na mashine. Hata hivyo, kazi za matengenezo zimesita kwa sasa kutokana na Shirika kukabiliwa na changamoto ya uhaba wa kifedha.

94. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa meli ya Mafuta ya MT Ukombozi II, kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 meli hii imefanyiwa marekebisho kama ilivyoanishwa katika mkataba *Warranty Period.* Marekebisho hayo yamefanywa na wataalamu kutoka Kampuni ya Damen Shipyard ambayo ndio Mjenzi wa meli hiyo.

95. **Mheshimiwa Spika,** Meli ya MT Ukombozi ambayo husafirisha mafuta kuja Zanzibar, kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, imefanya safari 11 kwa Unguja na Pemba na safari kumi zimefanyika Dar es Salaam.

Vile vile Shirika linaendelea kutoa huduma za uwakala wa meli. Hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya meli 202 za kigeni zimehudumiwa kwa kipindi hichi cha miezi tisa.

**Mapato na Matumizi**

**96.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya TSH 23,729,974,696 na hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH 7,314,068,446 zimekusanywa sawa na asilimia 31 ya makadirio ya bajeti. Kwa upande wa matumizi, Shirika lilipanga kutumia jumla ya TSH 23,636,749,478 kwa kazi za kawaida na Maendeleo na hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya TSH 8,843,605,560 zilitumika sawa na asilimia 37 ya makadirio ya bajeti.

**MALENGO YA SHIRIKA LA MELI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**97.** **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Lengo kubwa la Shirika ni kuliimarisha ili liweze kujiendesha kibiashara na kutoa huduma kwa jamii kwa kutumia meli zake zilizopo. Kwa upande wa uwakala, Shirika limepanga kuhudumia jumla ya meli 308 zikiwemo za makontena, mizigo mchanganyiko na meli za mafuta. Aidha, Shirika limepanga kuajiri wataalamu mbalimbali wanaohusiana na uendeshaji na usimamizi wa biashara za meli pamoja na kutoa mafunzo kwa wahandisi, mabaharia na waongoza meli wa Shirika.

**Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2021/2022**

**98.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Shirika limepanga kukusanya jumla ya TSH 15,642,893,880

na kutumia jumla ya TSH 11,740,173,679 kwa kazi za kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, jumla ya TSH 9,597,138,679 kwa kazi za kawaida na TSH 2,143,035,000 kwa kazi za maendeleo.

## C.3. MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR.

**99. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri Baharini ina jukumu la kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya baharini pamoja na uhifadhi wa mazingira ya baharini, kusimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli, utoaji wa leseni kwa Kampuni zinazojishughulisha na utoaji wa huduma bandarini na baharini, utoaji wa leseni kwa vyombo vidogo vidogo, utoaji wa leseni za manahodha na wahandisi wa vyombo vidogo vidogo, utoaji wa hati na vitambulisho vya mabaharia pamoja na kuidhinisha (endorsement) vyeti vya mabaharia. Aidha, Mamlaka ina jukumu la kusimamia usalama wa bandari zilizopo Zanzibar ikiwa ni utekelezaji wa Kanuni na Miongozo ya Kimataifa na Kikanda, kudhibiti safari za vyombo vya baharini, uchunguzi wa ajali za baharini, uratibu wa shughuli za utafutaji na uokozi kwa ajali za baharini pamoja na usimamizi wa maslahi ya mabaharia.

**100. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Mamlaka ilisajili meli tatu zenye uzito wa GRT 638 kwa usajili wa ndani (Tanzania Zanzibar Registry). Aidha, Mamlaka ilitoa leseni 416 kwa vyombo vidogo vidogo, leseni 320 za manahodha, leseni nane kwa Wahandisi (Boat Engineer) na kutoa vitabu vya Mabaharia (Discharge Book) 374 pamoja na mikataba 62. Vilevile, Mamlaka imeidhinisha vyeti 109 vya mabaharia

wanaosafiri na meli za nje kupitia kampuni ya DANAOS, pamoja na kuthibitisha vyeti vya mabaharia 334 (endorsement) wanaofanya kazi katika meli zilizosajiliwa kupitia usajili wa Tanzania Kimataifa.

**101. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri Baharini ilitoa jumla ya leseni 123 katika kipindi cha Julai, 2020 - Machi, 2021. Kati ya leseni hizo, leseni 58 zimetolewa kwa Mawakala wa utoaji wa mizigo Bandarini, leseni 15 kwa ajili "Jetty Installation", leseni 24 kwa vituo vya uzamiaji, leseni nne kwa vyombo vya starehe, leseni saba kwa vyombo vya michezo baharini, leseni nane kwa hoteli zinazoelea baharini, leseni mbili kwa michezo ya kite na leseni tano kwa kampuni zinazomiliki meli moja.

**102. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ilikagua jumla ya meli 41 za ndani zenye jumla ya GRT 38,714.98. Kati ya meli hizo, meli 19 zenye jumla ya GRT 18,079.14 zilifanyiwa ukaguzi wa kiusalama wa mwaka, meli 9 zenye GRT 10,396.00 zilifanyiwa ukaguzi wa dharura, meli 8 zenye GRT 2,409.73 zilifanyiwa ukaguzi wa kushitukiza na meli 5 zenye GRT 7,829.91 zilifanyiwa ukaguzi wa chelezoni.

**Mapato na Matumizi**

**103. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ilipanga kukusanya jumla TSH 3,350,419,962 na hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH 1,916,803,349 zimekusanywa sawa na asilimia 57 ya makadirio ya bajeti.

**104. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi, Mamlaka ilipanga kutumia jumla TSH 3,335,462,280. Hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH 1,547,046,485 zimetumika

sawa na asilimia 46 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 1,044,272,203 zimetumika kwa ajili ya mishahara na TSH 502,774,282 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

**MALENGO YA MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**105. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022, Mamlaka imepanga kuupitia na kuutekeleza Mpango Mkakati wa Mamlaka, kuendelea kuzifanyia mapitio Sheria pamoja na kutayarisha Miongozo na Kanuni mpya ili ziweze kuendana na matakwa ya Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Bahari Duniani (IMO). Aidha, Mamlaka imepanga kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali ili waweze kutekeleza majukumu yao kiufanisi.

**Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2021/2022**

**106. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022, Mamlaka ya Usafiri Baharini imekadiria kukusanya jumla ya TSH 3,502,412,000 na imepanga kutumia jumla ya TSH 3,468,054,000 kwa matumizi ya kawaida na Mishahara.

## C.4. MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR

**107. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaendelea na kazi zake za msingi za kuviendesha, kuvisimamia na kuvitunza Viwanja vya Ndege vya Serikali

pamoja na kusimamia usalama wa safari za abiria, ndege na mizigo katika Viwanja hivyo.

**108. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi, 2021, Mamalaka ya Viwanja vya Ndege imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:- kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 19 na mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 207 katika kada tofauti. Vilevile, Mamlaka imefanikiwa kuzifanyia matengenezo mashine tatu za ukaguzi wa mizigo ya abiria kwa lengo la kuimarisha usalama katika Viwanja vya Ndege vya Zanzibar. Kati ya mashine hizo, mashine mbili zimetengenezwa katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA na mashine moja katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. Aidha, Mamlaka imeongeza CCTV Camera tano katika Jengo la abiria (Terminal II) katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA. Pia, Mamlaka imeendelea na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigunda uliopo Nungwi kwa kuweka lami ya maji katika barabara ya kurukia na kutulia ndege yenye urefu wa mita 1,200 pamoja na kujenga jengo la ofisi za utawala.

**TAKWIMU ZA ABIRIA, MZIGO NA SAFARI ZA NDEGE**

**109. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Mamlaka imehudumia jumla ya safari za ndege 32,660 ikilinganishwa na safari 50,768 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020 sawa na upungufu wa asilimia 36 uliosababishwa na mripuko wa janga la maradhi ya COVID-19 ambapo baadhi ya nchi zililazimika kusitisha safari za ndege. Kati ya safari hizo, safari za ndege 26,822 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume na safari

za ndege 5,838 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. Kati ya safari hizo, safari za ndege 3,819 zikiwa ni safari za kimataifa na safari za ndani ni 28,841. **Kiambatanisho namba 6** kinahusika.

**110. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka pia imehudumia abiria 741,043 katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 ikilinganishwa na abiria 1,220,891 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020 sawa na upungufu wa asilimia 39. Abiria 673,562 walihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume na abiria 67,481 walihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. Kati ya abiria hao, abiria 446,757 wakiwa ni wa safari za kimataifa na 294,286 ni wa safari za ndani. Jumla ya Abiria waliopita (transit) ni 91,764 ambapo 88,704 walipita katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume na abiria 3,060 walipita katika Uwanja wa Ndege wa Pemba.

**111. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mizigo, Mamlaka imehudumia jumla ya tani 1,689 katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 ikilinganishwa na mzigo tani 1,873 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/2020 sawa na upungufu wa asilimia 10.

**112. Mheshimiwa spika,** Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2020/2021, imehudumia jumla ya Kampuni za ndege 57 katika Viwanja vya Ndege vya Zanzibar.

**Mapato na Matumizi**

**113. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilipanga kukusanya jumla ya TSH 20,902,316,407 kupitia

vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH 12,342,768,322 zimekusanywa sawa na asilimia 59 makadirio ya Mwaka.

114. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi, Mamlaka ilipanga kutumia jumla ya TSH 20,902,316,407. Kati ya fedha hizo, TSH 15,536,599,753 ni kwa kazi za kawaida na TSH 5,365,716,655 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2021, jumla ya TSH 10,337,293,556 zimetumika sawa na asilimia 49 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo TSH 5,002,815,379 mishahara na TSH 4,066,570,102 kwa ajili ya kazi za kawaida na TSH 1,267,908,074 kwa kazi za maendeleo.

## MALENGO YA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

115. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022, Mamlaka imepanga kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama ili kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa kwa kuwapatia wafanyakazi 162 mafunzo ya ulinzi na usalama katika fani mbali mbali pamoja na kuvipatia viwanja vya ndege mashine mpya tano za ukaguzi wa abiria na mizigo, kuendelea na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigunda kwa kuimarisha miundombinu ya njia za kurukia na kuegesha ndege na kuweka uzio, uwekaji wa taa za kuongozea ndege (precession lights) katika mfumo wa ILS kwa ajili ya kumuongoza rubani (wakati wa mvua, usiku au mawingu pamoja na kuimarisha mazingira ya kibiashara katika Uwanja wa AAKIA, Pemba na Kigunda kwa kuyashajihisha Mashirika ya Ndege yaanzishe safari

na kuendelea na safari zao Zanzibar. Aidha, Mamlaka imepanga kuhudumia abiria 1,865,928, Ndege 80,775 na Mzigo tani 3,344 kwa upande wa Uwanja wa Abeid Amani Karume na abiria 155,256 na Ndege 12,109 kwa Pemba

**Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2021/2022**

**116. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekadiria kukusanya jumla ya TSH 27,652,519,234 kupitia vyanzo vyake vya ndani na imepanga kutumia jumla ya TSH 27,652,519,234. Kati ya hizo, TSH 23,938,171,910 kwa kazi za kawaida na 3,714,347,324 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

## D. MASHIRIKIANO NA TAASISI ZA MUUNGANO

**117. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imeendelea kushirikiana na Taasisi za Muungano zilizopo hapa Zanzibar katika utoaji wa huduma na usimamizi wa Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji. Miongoni mwa Taasisi hizo ni Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Tanzania (TCAA), Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Tanzania (TMA), Mamlaka ya Mawasiliano ya Tanzania (TCRA), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Shirika la Posta la Tanzania (TPC), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC). Mashirikiano na Taasisi hizo yamechangia sana kukuza Sekta ya Usafiri na Mawasiliano hapa Zanzibar.

**118. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kuimarisha mahusiano mazuri na Taasisi hizo, imefanya vikao vya ushirikiano na Wizara/Taasisi hizo kwa lengo la kubadilishana uzoefu utakaosaidia kuimarisha na kuweka mikakati itakayoimarisha utoaji wa huduma pamoja na kukuza ushirikiano. Napenda kuchukua nafasi hii kuzipongeza Taasisi hizo kwa kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na nachukua fursa hii kuzitaka ziendeleze ushirikiano huo kwa maslahi mapana ya Nchi yetu.

## E. MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KATIKA SEKTA YA USAFIRISHAJI NA MAWASILIANO.

**119. Mheshimiwa Spika,** sekta binafsi imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kusaidia juhudi za Serikali za kuendeleza na kuimarisha usafiri wa Anga, Baharini na Nchi kavu pamoja na huduma za Mawasiliano hapa Zanzibar. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi inatambua na kuthamini mchango wa sekta binafsi katika kujenga uchumi wa nchi yetu kwa kutoa huduma bora zenye kufanikisha sekta nyengine za kiuchumi na kijamii, kuchangia Pato la Taifa na kutoa ajira kwa wananchi. Wizara itaendelea kuhamasisha na kuweka mazingira mazuri ya kisera kwa sekta hiyo ili iendelee kuimarisha huduma za Usafiri na Mawasiliano hapa Zanzibar.

**120. Mheshimiwa Spika,** nachukua nafasi hii kuzipongeza Taasisi binafsi zinazotoa huduma za Usafirishaji na Mawasiliano kwa kazi nzuri wanayoifanya na naziomba ziendelee kushirikiana na Serikali katika kuwahudumia wananchi.

## F. MUELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA KILA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

121. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji kwa kila programu zinazosimamiwa na Wizara pamoja na Taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Wizara kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, naomba kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

122. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ina jukumu la kusimamia sekta mbili kuu hapa Zanzibar ambazo ni Sekta ya Mawasiliano na Sekta ya Usafirishaji. Kwa kuzingatia Sekta hizo, Wizara ina Programu Kuu tatu (3) ambazo ni:- Programu ya Miundombinu na Huduma za Usafirishaji, Programu ya Miundombinu na Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) pamoja na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

## G. VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

123. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi katika kuimarisha huduma za Mawasiliano na Usafirishaji hapa Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2021/2022, imeweka vipaumbele katika kuimarisha miundombinu ya usafirishaji na huduma za mawasiliano kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo 2050 (Vision 2050), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025 pamoja

na ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alizozitoa wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2020. Katika kuweka vipaumbele hivyo, Wizara imezingatia vipaumbele vikuu vya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ikiwemo kuimarisha miundombinu ya usafiri wa anga kwa kuanza maandalizi ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba, kuendeleza ujenzi wa Uwanja mdogo wa Kigunda uliopo Nungwi, kuweka mtambo wa kuongozea ndege (Instrument Landing System - ILS) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume na kuanza maandalizi ya ujenzi wa Bandari Shirikishi ya Mangapwani (Mizigo, Uvuvi, Chelezo, Mafuta na Gesi).

**124. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imepanga kuimarisha miundombinu ya barabara ikiwemo kuendelea na ujenzi wa barabara mbali mbali ambazo ujenzi wake umeanza katika bajeti zilizopita. Barabara hizo ni: Barabara ya Jozani – Charawe – Ukongoroni - Bwejuu (km 23), Barabara ya Wete – Chake (km 22.1), Barabara ya Kizimbani – Kiboje (km 7.2), Barabara ya Finya – Kicha (km 8.8), Barabara ya Micheweni – Kiuyu – Maziwang'ombe (km 7) pamoja na maandalizi ya Ujenzi wa Daraja la Uzi – Ng'ambwa (km 2.2).

## H. MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU NA MALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**125. Mheshimiwa Spika,** programu kuu zilizotajwa hapo juu zimewekewa malengo makhususi, matokeo ya muda mrefu

yatakayopatikana, huduma zitakazotolewa, shabaha na viashiria mbali mbali vitakavyotumika kupima utekelezaji wa huduma zitakazotolewa katika Sekta ya Mawasiliano na Sekta ya Usafirishaji. Maelezo ya programu na malengo yake ambayo yatatekelezwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ni kama ifuatavyo:

## H.1. PROGRAMU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI.

**126. Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuwepo kwa miundombinu bora na huduma za usafiri zilizo bora, salama na endelevu. Programu ya Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ina programu ndogo mbili (2) ambazo ni; Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji na Programu Ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji.

### H.1.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji

**127. Mheshimiwa Spika,** programu hii ndogo inasimamiwa na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani pamoja na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar. Programu hii ina lengo la kuhakikisha huduma bora za usafiri wa barabara zilizo salama zinapatikana muda wote. Huduma zinazotolewa katika programu hii ni usimamizi wa utoaji wa huduma za usafiri wa barabara pamoja na matengenezo ya vyombo vya moto.

**128. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara kupitia Taasisi zinazosimamia programu hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

**MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI - ZANZIBAR**

129. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji imepanga kuimarisha usalama wa barabarani kwa kuendelea kuwapatia elimu watumiaji wote wa barabara na kuimarisha mfumo wa ukaguzi wa vyombo vya moto. Aidha, Mamlaka imepanga kuimarisha mfumo wa utoaji wa huduma za usafiri barabarani kwa njia ya kielektroniki ili kuenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia pamoja na kuondoa usumbufu kwa wananchi wanaohitaji huduma hizo.

130. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imepangiwa kukusanya jumla ya TSH 3,400,585,000 kupitia vyanzo vyake vya mapato.

**WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR**

131. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2021/2022, imepanga kuvifanyia matengenezo vyombo vya moto 1200 vya Serikali na binafsi, kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya utengenezaji wa gari, kuongeza vitendea kazi pamoja na kulifanyia matengenezo jengo la Ofisi yake iliyopo Chumbuni.

132. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji inaombewa kutumia jumla ya TSH 3,266,100,000 kwa kazi za kawaida

na mishahara. Kati ya fedha hizo, TSH 1,371,800,000 ni ruzuku kwa ajili ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani na TSH 1,894,300,000 ni Ruzuku kwa ajili ya Wakala Karakana Kuu ya Magari Zanzibar.

### H.1.2. Programu Ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji

133. **Mheshimiwa Spika,** programu hii itasimamiwa na Wakala wa Barabara Zanzibar na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Programu hii ina lengo la kuwepo miundombinu ya usafirishaji iliyo bora, salama na endelevu kwa Unguja na Pemba. Huduma zinazotolewa katika programu hii ni utunzaji na utengenezaji wa barabara, uimarishaji wa miundombinu ya barabara ikiwemo miradi mikubwa ya ujenzi, uimarishaji wa miundombinu ya usafiri wa anga na uimarishaji wa miundombinu ya usafiri wa baharini.

134. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara kupitia Taasisi zinazosimamia programu hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

### WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR (ZANROADS)

135. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia Programu Ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji imepanga kuzijenga na kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali kwa kiwango cha lami Unguja na Pemba zitakazogharamiwa na Mfuko wa Barabara Zanzibar ikiwemo ujenzi wa Barabara ya Kinduni – Kichungwani - Kitope (km4), matengenezo ya Barabara ya Biziredi – Mlandege - Mbuyu Taifa - Gulioni (km1.3), Barabara ya Mlandege - Darajani (km 0.6),

Barabara ya Kipapo - Mgelema - Wambaa (km 9.3) pamoja na uwekaji wa taa za kuongozea gari kwenye makutano ya Barabara Kwajuma Pweza na makutano ya Barabara Kiembesamaki /Barabara ya Mkapa.

**136. Mheshimiwa Spika,** Wakala itaendelea kuzitunza barabara mbali mbali zilizokwisha kujengwa kwa kuzifanyia usafi pamoja na matengenezo kwa kujenga misingi ya uondoaji wa maji ya mvua barabarani, kuimarisha barabara za mijini kwa kujenga njia za waendao kwa miguu, kuimarisha maeneo ya makutano ya barabara kuu pamoja na kuimarisha alama za barabarani. Orodha ya barabara ambazo zimepangwa kufanyiwa matengenezo Unguja na Pemba kwa mwaka wa fedha 2021/2022 zinaonekana katika **Kiambatanisho namba 7.**

**137. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara imepanga kutumia jumla ya TSH 12,862,000,000 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara mbali mbali Unguja na Pemba.

## IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

**138. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu Ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji itaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi mikubwa katika Sekta ya usafirishaji itakayogharimu jumla ya TSH 132,795,166,000. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa barabara mbali mbali Unguja na Pemba zenye urefu wa km 195.6, Ujenzi wa Daraja la Uzi Ng'ambwa lenye urefu wa km 2.2, pamoja na maandalizi ya ujenzi wa Bandari Shirikishi ya Mangapwani. Orodha

ya miradi inayotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 inaonekana katika **Kiambatanisho Namba 8.**

**139.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu Ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji inaombewa kutumia jumla ya TSH 136,699,766,000 kwa kazi za kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, TSH 3,904,600,000 ni ruzuku kwa kazi za kawaida kwa ajili ya Wakala wa Barabara Zanzibar na TSH 132, 795,166,000 zitatumika kwa kazi za maendeleo, ikiwa TSH 16,804,166,000 mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TSH 115,991,000,000 ni mchango kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## H.2. PROGRAMU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA).

**140.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Zanzibar. Programu hii ina programu ndogo mbili (2) ambazo ni; Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA pamoja na Usimamizi wa Huduma za TEHAMA.

### H.2.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA

**141.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar (ZICTIA) na ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu bora ya mawasiliano iliyo salama na endelevu. Huduma zinazotolewa katika programu hii ndogo ni usimamizi wa matumizi ya Mkonga wa Taifa wa mawasiliano, kituo cha

kuhifadhia taarifa za kielektroniki (Data Center) pamoja na minara ya mawasiliano ya simu.

**142. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara kupitia Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA imepanga kuimarisha huduma ya Mkonga kwa kuusambaza km 56 za Mkonga wa Mawasiliano katika maeneo ambayo yana wateja wengi ambao wanahitaji huduma hiyo (*Carrier to Carrier fiber Network Optimization*), kuongeza njia mbadala za Mkonga wa Mawasiliano (Backborne Expansion) zikiwemo njia ya Mahonda - Kinyasini na Amani – Dunga pamoja na kufanya matengenezo ya vituo vya kusimamia Mkonga (Point of Presence - POP).

**143. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar imepanga kuimarisha kituo kilichopo cha kuhifadhia taarifa (Data Center) kwa kuondoa vifaa chakavu na kuweka miundombinu mipya na ya kisasa itakayowezesha Mashirika na Taasisi za Serikali kuweza kuhifadhi taarifa zao pamoja na kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu yatakayosaidia kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Vilevile, Wakala imepanga kuhakikisha upatikanaji wa mawasiliano salama kwa taasisi za Serikali kwa kuzipatia mtandao (internet) wa uhakika na wa kutosha pamoja na kuziunganisha taasisi mbalimbali za Serikali na mawasiliano salama ya simu na mitandao (voice over IP).

**144. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA inaombewa kutumia jumla ya TSH 2,210,500,000

kwa matumizi ya kawaida ambazo ni Ruzuku kwa ajili ya Wakala wa Miundmbinu ya TEHAMA Zanzibar (ZICTIA).

**145. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara kupitia Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar imepangiwa kukusanya jumla ya TSH 2,326,533,000 kupitia vyanzo vyake vya mapato.

### H.2.2. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Huduma za TEHAMA

**146. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Mawasiliano na ina lengo la kuhakikisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano yanaongezeka kwa taasisi zote pamoja na jamii. Huduma zinazotolewa katika programu hii ndogo ni kusimamia upatikanaji wa huduma bora za TEHAMA Zanzibar.

**147. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara kupitia programu hii ndogo imepanga kusimamia huduma mbalimbli za mawasiliano kama vile posta, simu na intaneti pamoja na kuendelea kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa jamii kupitia Vituo vya TEHAMA Jamii vilivyopo katika Wilaya za Unguja na Pemba. Aidha, Wizara inaendelea na ujenzi wa kituo cha "Call Center" kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) pamoja na kuendeleza uwekaji wa Anuani za Makaazi na Postikodi katika Mitaa ya Unguja na Pemba.

**148. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Huduma za TEHAMA inaombewa kutumia jumla ya TSH 1,304,275,000 kwa kazi za kawaida na mishahara.

## H.3. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA.

**149. Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inaratibu na kutayarisha Sera na Mipango bora katika Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii ina programu ndogo tatu (3) ambazo ni; Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara pamoja na Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba.

### H.3.1. Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji

**150. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na ina lengo la kuimarisha huduma za ofisi na usimamizi wa rasilimali watu katika Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji. Huduma zinazotolewa katika programu hii ni ununuzi wa vifaa mbalimbali vya ofisi pamoja na kusimamia shughuli za kiutawala na utumishi katika Wizara.

**151. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara kupitia Programu hii imepanga kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili waweze kutoa huduma bora na kwa ufanisi pamoja na kuimarisha huduma za kiutawala na utumishi ikiwemo kuweka mazingira mazuri ya kazi, kusimamia maslahi ya watumishi pamoja na kuongeza vitendea kazi kwa lengo la kuleta ufanisi.

**152. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji inaombewa kutumia jumla ya TSH 2,310,366,000 ambazo zitatumika kwa kazi za kawaida na mishahara.

### H.3.2. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

**153. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na ina lengo la kuhakikisha Mipango na Sera mbali mbali za Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji zinatayarishwa pamoja na kufuatilia utekelezaji wake. Huduma zinazotolewa katika programu hii ni utayarishaji na utekelezaji wa Bajeti pamoja na uandaaji na uibuaji wa sera na tafiti za Wizara.

**154. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara kupitia Programu hii imepanga kuendelea kuratibu na kufanya Tafiti za Wizara, kuzifanyia mapitio Sera ya Usafiri ya mwaka 2008 na Sera ya TEHAMA ya mwaka 2013 ili ziendane na mahitaji ya sasa. Vilevile, Idara imepanga kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo, kukusanya takwimu mbali mbali katika sekta zinazosimamiwa na Wizara, kutayarisha mpango wa ufuatiliaji na tathmini wa kazi za Wizara (Monitoring and Evalution Frame Work), kuratibu taasisi na mashirika yanayojitegemea yaliyo chini ya Wizara, kuratibu na kufanya vikao vya ushirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ), Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (SMT). Aidha, Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kutoa mafunzo kwa watendaji wake yanayohusiana na utayarishaji wa bajeti katika mfumo wa programu (PBB), ufuatiliaji na tathmini, namna ya kufanya tafiti pamoja na usimamizi wa miradi kwa lengo la kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao.

**155. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara inaombewa kutumia jumla ya TSH 801,336,000 kwa kazi za kawaida na mishahara.

### H.3.3. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

**156. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Ofisi Kuu Pemba na ina lengo la kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatekelezwa kwa upande wa Pemba. Huduma inayotolewa katika programu hii ndogo ni uratibu wa kazi za Wizara Pemba ikiwemo kusimamia shughuli za utawala na utumishi, mipango na bajeti, huduma za usafiri barabarani, huduma za TEHAMA pamoja na ujenzi, utunzaji na matengenezo ya barabara mbali mbali – Pemba. Aidha, Ofisi Kuu Pemba imepanga kuweka mazingira bora ya Ofisi kwa kufanya matengenezo makubwa ya jengo la Ofisi lililopo Chake Chake na nyumba za Wizara zilizopo Pandani pamoja na Gombani.

**157. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba inaombewa kutumia jumla ya TSH 1,003,222,000 kwa kazi za kawaida na mishahara.

## I. HITIMISHO

**158. Mheshimiwa Spika,** kabla sijamaliza hotuba yangu hii sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na ustahamilivu wakati wote nilipokua nikitoa maelezo ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano

na Uchukuzi. Ni matumaini yangu kwamba Baraza lako Tukufu litatoa michango ambayo itasaidia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kutatua changamoto mbali mbali ambazo zilijitokeza katika kipindi cha mwaka 2020/2021 na hatimae kuipitisha bajeti hii kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Wizara zilizopangwa katika programu zake kuu tatu (3) kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

159. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ambayo nimeyaeleza katika hotuba hii ni matokeo ya ushirikiano wa wahusika mbali mbali wa ndani na nje ya Nchi. Kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi napenda kuchukua fursa hii kuzitambua, kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi mbali mbali tulizoshirikiana nazo katika kuendeleza sekta za Wizara hii. Shukurani za dhati ziende kwa Washirika wa Maendeleo wakiwemo Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi Afrika (BADEA), Exim Benki ya China, Saudi Fund na Mfuko wa Maendeleo ya Nchi zinazotoa Mafuta kwa wingi Duniani (OFID).

160. **Mheshimiwa Spika**, vile vile, natoa shukurani zangu kwa Taasisi binafsi zinazotoa huduma za mawasiliano na usafirishaji hapa Zanzibar ikiwemo Kampuni za mawasiliano za Zantel, Tigo, Halotel, Airtel, Vodacom, TTCL na Zanlink. Kampuni za usafirishaji wa baharini ikiwemo African Shipping Cooperation, Kilimajaro Fast Ferries Marine Services Limited, Azam Marine na Zanzibar Fast Ferries. Kwa upande wa usafiri wa anga tunazipongeza

Kampuni za Air Tanzania, Assalam Air, Costal Travel, Auric Air, Pelican Air, Precission Air, Zan Air, Flight link, Tropical Air na Kampuni za Kimataifa ikiwemo Ethiopian Airlines, Turkish Airlines, Meridiana, Qatar Airlines, Fly Dubai, Kenya Airways, Oman Air, Fly Mango, Condor Air, Israil Airlines, Rossiya, KLM, 540 Aviation, Uganda Air, Air Italy na nyenginezo.

161. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru kwa dhati Katibu Mkuu Ndugu Amour Hamil Bakari, Afisa Mdhamini, Wakurugenzi, Wakurugenzi Wakuu wa Mashirika na Taasisi pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa ushirikiano na juhudi wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nawashukuru wale wote ambao walichangia katika kutayarisha hotuba hii.

## J. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022.

162. **Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuiwezesha Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kutekeleza majukumu na malengo yake yaliyoainishwa katika Programu Kuu tatu (3) katika hotuba hii pamoja na utekelezaji wa Ilani Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **TSH 147,595,566,000** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

163. **Mheshimiwa Spika,** kati ya fedha hizo **TSH 14,800,400,000** ni kwa ajili ya kazi za kawaida, **TSH**

**16,804,166,000** ni mkopo kutoka kwa Washirika wa maendeleo na **TSH 115,991,000,000** ni fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**164.** **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe makusanyo ya **TSH 5,727,118,000** kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**165.** **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.



**Mheshimiwa Rahma Kassim Ali (MBM)**
**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar**

# VIAMBATANISHO:

### Kiambatanisho Namba 1A: Ukaguzi wa Vyombo vya Moto Julai 2020 - Machi 2021

| Aina ya Chombo | Ukaguzi wa kawaida | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Unguja | Pemba | |
| Gari | 18,395 | 3,419 | **21,814** |
| Vyombo vya maringi mawili | 12,437 | 2,303 | **14,740** |
| **Jumla** | **30,832** | **5,722** | **36,554** |

### Kiambatanisho Namba 1B: Ruhusa za Njia na Usafirishaji Julai 2020 - Machi 2021

| Sehemu ilipotolewa | Aina ya Huduma iliyotolewa | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Daladala | Shamba | P/Hire | Taxi | Mizigo A | Mizigo C | School | Staff bus | Kukodisha | Jumla |
| **Unguja** | 1,198 | 909 | 2,023 | 349 | 1,487 | 2,728 | 98 | 72 | 55 | 8,919 |
| **Pemba** | 17 | 429 | 137 | 30 | 161 | 419 | 12 | 02 | 00 | 1,207 |
| **Jumla** | **1,215** | **1,338** | **2,160** | **379** | **1,648** | **3,147** | **110** | **74** | **55** | **10,126** |

### Kiambatanisho Namba 1C: Utoaji wa leseni kwa madereva wanafunzi kwa kipindi cha Julai 2020 - Machi 2021

| Sehemu ilipotolewa | Leseni za madereva wanafunzi zilizotolewa | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | A | B1 | B | C1 | C | D1 | D | E | M | G | SMZ | Jumla |
| Unguja | 2,072 | 3,098 | 01 | 326 | 87 | 215 | 243 | 05 | 70 | 00 | 19 | **6,136** |
| Pemba | 614 | 262 | 12 | 61 | 12 | 56 | 13 | 00 | 00 | 00 | 00 | **1,030** |
| **Jumla** | **2,686** | **3,360** | **12** | **387** | **99** | **271** | **256** | **5** | **70** | **0** | **19** | **7,166** |

**Kiambatanisho namba 2: Orodha ya Taasisi zilizoungwanishwa na Mkonga wa Mawasiliano kwa kipindi cha Julai, 2020 – Machi, 2021.**

| Na | Jina la Taasisi |
|---|---|
| | **Unguja** |
| 1 | Nyumba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar - Migombani |
| 2 | Nyumba ya Makamo wa Pili wa Rais -Mazizini |
| 3 | Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi A |
| 4 | Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar - Mwera |
| 5 | Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar - Koani |
| 6 | Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar -Makunduchi |
| 7 | Studio ya muziki Rahaleo -Zanzibar |
| 8 | Tume ya Utangazaji Zanzibar |
| 9 | Kituo cha usimamizi wa miji salama Zanzibar (eCTV )- Maisara |
| 10 | Kituo cha usimamizi wa miji salama Zanzibar (eCTV )- Wete |
| 11 | Kituo cha usimamizi wa miji salama Zanzibar (eCTV )- Chake Chake |
| 12 | Kituo cha usimamizi wa miji salama Zanzibar (eCTV )- Mkoani |
| 13 | Kituo cha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar - Mnazimmoja |
| 14 | Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A |
| 15 | Ofisi ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale |
| 16 | Ofisi ya Manispaa ya Wilaya ya Magharibi B |
| 17 | Idara ya Watu wenye Ulemavu |
| 18 | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) |
| 19 | Kampuni ya Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC) |
| 20 | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar |
| 21 | Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA) |
| 22 | Idara ya Nishati - Zanzibar |

| | |
|---|---|
| 23 | Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar |
| | **Pemba** |
| 24 | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA) - Wete |
| 25 | Wakala wa Majengo - ChakeChake |
| 26 | Baraza la Mji - Mkoani |
| 27 | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) - Gombani |
| 28 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) - Hospitali ya Wete |

**Kiambatanisho Namba 3A: Wafanyakazi waliopatiwa mafunzo ya muda mrefu kwa mwaka wa fedha 2020/2021**

| Na | Programu Ndogo | Shahada ya Uzamivu | | Shahada ya Uzamili | | Shahada ya Kwanza | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mke | Mme | Mke | Mme | Mke | Mme | |
| 1 | Mawasiliano | - | 1 | - | - | - | - | **1** |
| 2 | Utawala na Uendeshaji | - | - | - | - | 1 | 2 | **3** |
| 3 | Mipango na Sera | - | - | 1 | - | - | - | **1** |
| | **Jumla Kuu** | | **1** | **1** | **-** | **2** | **2** | **5** |

**Kiambatanisho Namba 3B: Wafanyakazi waliopatiwa mafunzo ya muda mfupi kwa mwaka wa fedha 2020/2021**

| Na. | Programu Ndogo | W/Ke | W/Me | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Utawala na Uendeshaji | - | - | **-** |
| 2 | Mipango na Sera | - | - | **-** |
| 3 | Mawasiliano | 3 | 10 | **13** |
| 4 | Kuratibu Shughuli za Wizara Pemba | - | - | **-** |
| | **Jumla Kuu** | **3** | **10** | **13** |

**Kiambatanisho Namba 4: Matumizi ya kawaida na maendeleo kwa kila programu kwa kipindi cha Julai 2020 - Machi 2021**

| Na. | Programu Kuu/ Programu Ndogo | Makadirio 2020/2021 | Matumizi Halisi Julai 2020 hadi Machi 2021 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **Programu ya Miundombinu na Huduma za Usafirishaji** | | | |
| 1.1 | Usimamizi wa Usafirishaji | 2,186,900,000 | 952, 681,372 | 43.5 |
| 1.2 | Miundombinu ya Usafirishaji | 178,315,073,000 | 50,720,204,945 | 28.4 |
| 1.3 | Huduma za Usafirishaji | 2,500,000,000 | - | - |
| | **Jumla ya Programu Kuu** | **183,001,973,000** | **51,672,886,317** | **28.2** |
| **2.** | **Programu ya Miundombinu na Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)** | | | |
| 2.1 | Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA | 1,760,000,000 | 553,530,835 | 31 |
| 2.2 | Usimamizi wa Huduma za TEHAMA | 1,300,000,000 | 284,574,351 | 22 |
| | **Jumla ya Programu Kuu** | **3,060,000,000** | **838,105,186** | **27.3** |
| **3** | **Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi** | | | |
| 3.1 | Utawala na Uendeshaji | 2,780,000,000 | 875,838,394 | 32 |
| 3.2 | Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara | 924,000,000 | 224,485,390 | 24 |
| 3.3 | Uratibu wa Shughuli za Wizara – Pemba | 1,210,000,000 | 431,478,400 | 35.6 |
| | **Jumla ya Programu Kuu** | **4,914,000,000** | **1,531,802,184** | **31.1** |
| | **Jumla Kuu ya Programu Kuu za Wizara** | **190,975,973,000** | **54,042,793,687** | **28.2** |

**Kiambatanisho Namba 5: Mapato yaliyokusanywa kwa Kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021**

| Na | Taasisi /Idara. | Makadirio 2020/2021 | Fedha Zilizokusanywa Julai 2020 - Machi 2021 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Afisi Kuu Pemba | 866,500,000 | 239,367,000 | 27.6 |
| 2 | Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani | 2,534,085,000 | 1,863,184,400 | 73.5 |
| | **Jumla** | **3,400,585,000** | **2,102,551,400** | **61.8** |

**Kiambatanisho Namba 6: Idadi ya ndege zilizohudumiwa kwa kipindi cha Julai 2020 - Machi 2021**

| Na | Aina ya ndege | Idadi ya ndege | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Unguja | Pemba | |
| 1 | Ndege zenye ratiba (schedule) | 20,452 | 5,172 | **25,624** |
| 2 | Ndege zisizo na ratiba (charter) | 4,555 | 596 | **5,151** |
| 3 | Mizigo (cargo) | 46 | - | **46** |
| 4 | Binafsi (private) | 70 | - | **70** |
| 5 | Kijeshi (military) | 46 | 7 | **53** |
| 6 | Nyenginezo | 1,653 | 63 | **1,716** |
| | **JUMLA** | **26,822** | **5,838** | **32,660** |

**Kiambatanisho Namba 7: Orodha ya kazi za matengenezo ya Barabara zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kupitia Mfuko wa Barabara Zanzibar**

| Na. | Kazi za matengenezo ya barabara |
|---|---|
| | **Unguja** |
| **1.** | Ujenzi wa daraja eneo la Machui |
| **2.** | Ujenzi wa njia za waendao kwa miguu kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume hadi Mazizini kwenye makutano ya barabara ya kwenda ZRB (km2.5) |
| **3.** | Matengenezo ya barabara ya Biziredi – Mlandege – Mbuyutaifa - Gulioni (km1.3) na Mlandege - Darajani (km 0.6) kwa kiwango cha lami |
| **4.** | Matengenezo ya barabara Uwanja wa Tumbaku (Magereza) - Maktaba (km 0.4) kwa kiwango cha lami |

| | |
|---|---|
| **5.** | Uwekaji wa taa za kuongozea gari kwenye makutano ya barabara Kwajuma Pweza na makutano ya barabara Kiembesamaki (Mkapa road) |
| **6.** | Upembuzi Yakinifu na Usanifu barabara ya Mahonda - Pangatupu-Bumbwini (km8), Mahonda - Zingwezingwe (km7.6), Kituo cha Polisi Mwera - Fuoni Kibondemzungu (km 6.1) na uimarishaji wa misingi ya maji ya mvua barabara ya Kiembesamaki - Mtopepo (Mkapa road) |
| **7.** | Uzibaji wa mashimo kwenye barabara za lami |
| **8.** | Ukataji wa majani, usafishaji wa misingi, madaraja kwenye barabara za lami (km 439) |
| **9.** | Matengenezo (Overlaying) ya Barabara ya Kitogani – Paje (km 1.5) |
| **10.** | Kukamilisha ujenzi wa barabara ya Kinduni – Kichungwani -Kitope (km4) na Sharifumsa – Mwanyanya - Skuli ya Bububu (km 3.8) kwa kiwango cha lami. |
| | **Pemba** |
| **1.** | Ujenzi wa barabara ya Kipapo - Mgelema – Wambaa (km 9.3) kwa kiwango cha lami |
| **2.** | Ujenzi wa barabara za maeneo huru Micheweni (km 2.4) kwa kiwango cha lami |
| **3.** | Kufanya Upembuzi Yakinifu na Sanifu kwa barabara ya Machomane – Ndugukitu - ZBC (km3) |
| **4.** | Kufanya upembezi yakinifu na Usanifu wa Daraja la Chamanagwe lililoko kwenye barabara ya Ole - Konde |
| **5.** | Uzibaji wa mashimo kwenye barabara za lami |
| **6.** | Ukataji wa majani, usafishaji wa misingi na madaraja kwenye barabara za lami (km 266). |

**Kiambatanisho Namba 8: Orodha ya Miradi inayotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022**

| Jina la Mradi | | Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa fedha 2021/2022 | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | Mchango wa Washirika wa Maendeleo | Jumla |
| 1. | Ujenzi wa Barabara ya Kizimbani – Kiboje (km 7.2) | 9,291,000,000 | - | **9,291,000,000** |
| 2. | Ujenzi wa barabara ya Bububu- Mahonda - Mkokotoni, Matemwe-Muyuni, Pale – Kiongele, Bububu Polisi - Kwanyanya na Fuoni-Kombeni (km 54.5) | - | 7,100,000,000 | **7,100,000,000** |
| 3. | Ujenzi wa barabara ya Wete - Chake (km 22.1) | 8,000,000,000 | 9,704,166,000 | **17,704,166,000** |
| 4. | Ujenzi wa Barabara ya Fumba – Kisauni (km 12) | 1,000,000,000 | - | **1,000,000,000** |
| 5. | Ujenzi wa barabara ya Jozani – Charawe - Ukongoroni (km 23) | 18,000,000,000 | - | **18,000,000,000** |
| 6. | Ujenzi wa Daraja la Unguja Ukuu - Uzi Ng'ambwa (km 2.2) | 24,500,000,000 | - | **24,500,000,000** |
| 7. | Ujenzi wa barabara ya Jumbi Sokoni – Tunguu (km 4) | 11,200,000,000 | - | **11,200,000,000** |
| 8. | Ujenzi wa barabara ya Finya - Kicha (km 8.8) | 8,000,000,000 | - | **8,000,000,000** |
| 9. | Ujenzi wa barabara ya Konde – Msuka (km 4.2); Micheweni – Maziwa ng'ombe – Kiuyu (km 7.3 ) Mapofu – Shumba viamboni – Tumbe Bandarini (km 11); Micheweni – Shumba Mjini (km 3.5) na Mgagadu – Kwautao (km 5.6) | 11,000,000,000 | - | **11,000,000,000** |
| 10. | Ujenzi wa kilomita (km 30.5) za Misingi ya kuondoshea maji katika barabara | 5,000,000,000 | - | **5,000,000,000** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | Ujenzi wa barabara ya Bumbwini Skuli – Kiongwe (km 4.3); Mwera – Masingini – Bububu Kijichi (km 8); Mahonda – Pangatupu – Bumbwini (km 8), Mwera Polisi – Fuoni (km 6.1); Kama (km 3) na Darajabovu – Miembe saba (km 3.3) | 7,000,000,000 | - | **7,000,000,000** |
| 12. | Uimarishaji wa Uwanja wa ndege wa Pemba | 2,000,000,000 | - | **2,000,000,000** |
| 13. | Ujenzi wa Uwanja mdogo wa Kigunda | 8,000,000,000 | - | **8,000,000,000** |
| 14. | Ujenzi wa Bandari shirikishi ya Mangapwani | 3,000,000,000 | - | **3,000,000,000** |
| **Jumla Kuu** | | **115,991,000,000** | **16,804,166,000** | **132,795,166,000** |